SUMAIT University Journal (SUJ)
ISSN (2507-7864)
Issue No. 11 (Decembar 2022)

# AINA NA MBINU ZA UTOAJI MOTISHA YA NJE WAKATI WA UFUNDISHAJI KISWAHILI KWA WAGENI

Zuleikha Abdalla Rashid

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
zuleikha2014@gmail.com

*Received: 1 April 2022, Accepted: 23 June 2022, Published: December 2022*
*© SUMAIT University Journal 20222*

**Abstract**

*The article based on the provision of external motivation when teaching Kiswahili to foreigners. The article focused to investigate the types and methods of external motivation which is used in providing motivating Kiswahili for foreigners. Data was obtained from locally diary and structured observation methods, where six teachers from the State Universty of Zanzibar, in the depertment of Kiswahili for foreigners participated in providing information related to the topic of this article. The result have shown that there are two types of external motivation. Verbal external motivation, example; good, very good, excellent, fair, congratulation, mashaallah and all right. External practical motivation, example; clap and smile. The reseacher has also discovered that teachers who teach Kiswahili for foreigner use a variety of method in providing external motivation. Example method of praising students, using emoji, gift-giving method and congratulating method. The author recommends teachers to provide verbal and practical external motivation, they increase the student motivation to learn as well as used properly it brings success and good results in learning.*

***Key words: Motivation, external motivation, foreign language and foreign language learning.***

**Ikisiri**

*Makala hii imejikita katika utoaji motisha ya nje wakati wa ufundishaji Kiswahili kwa wageni. Makala imelenga kuchunguza aina na mbinu za utoaji motisha za nje zinazotumika katika ufundishaji Kiswahili kwa wageni. Mbinu ya shajara na ushuhudiaji ilitumika kukusanya data za uwandani ambapo walimu sita kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, katika Idara ya Kiswahili kwa Wageni walishiriki katika kutoa taarifa zinazohusiana na mada ya makala hii. Matokeo yalionesha kuna aina kuu mbili za motisha ya nje. Motisha ya nje zinazotumia maneno kama nzuri, nzuri sana, haijambo, hongera, mashaallahu, vyema kabisa pamoja na motisha ya nje zinazotumia vitendo kama kupiga kofi, alama ya nipe tano na kutabasamu. Aidha mtafiti aligundua walimu wanatumia mbinu ya kuwasifu wanafunzi, mbinu ya kutumia imoji, mbinu ya kutoa zawadi na mbinu ya kuwashajihisha kwa kuwapongeza wanafunzi katika utoaji motisha ya nje wakati wa ufundishaji Kiswahili kwa*

*wageni. Mwandishi anawasisitiza walimu kutumia motisha ya maneno na vitendo, kwani motisha hizo huongeza maradufu ari na hamu ya wanafunzi katika kujifunza. Vilevile, motisha ikitumika ipasavyo inaleta mafanikio na matokeo mazuri ya kujifunza.*

***Istilahi muhimu: Motisha, motisha ya nje, lugha ya kigeni na ufundishaji wa lugha ya kigeni***

**1.0 Utangulizi**

Suala la utoaji wa motisha lilianzia karne nyingi zilizopita katika masuala ya saikolojia. Wataalamu mbalimbali walihusisha utoaji wa motisha na mitazamo ya wanafunzi katika upatikanaji wa lugha ya pili ambayo huathiriwa na jamii husika. Utoaji wa motisha husaidia kumuhamasisha mtu kufanya jambo kwa lengo la kupata matokeo mazuri na kujifunza kwa ufanisi zaidi. Borah (2021) anaamini motisha ni jambo lenye ushawishi mkubwa katika hali ya ufundishaji na ujifunzaji. Utoaji wa motisha huwasukuma wanafunzi ili kufikia malengo yao ya kujifunza.
Hali hii husababisha hamasa inayotengenezwa kwa makusudi ili kuwafanya wanafunzi wavutike na jambo wanalolifanya haswa pale wanafunzi wanaposifiwa kwa vitendo ama maneno.

Utoaji wa motisha ya nje katika ufundishaji wa lugha ya pili ama lugha ya kigeni hufanyika kwa kuandaa mazingira mazuri ya kufundishia. Mwalimu anapaswa atengeneze mazingira ya urafiki darasani yenye utulivu na usalama. Mazingira hayo yataendeleza hali ya kirafiki ambayo wanafunzi wote watatambuliwa na kuthaminiwa. Reeve na Halusic (2009) wanaeleza kuwa, mwalimu ajaribu kupanga kazi za darasani ambazo zinahusiana kwa ukaribu na mahitaji, malengo, maadili na raghba za wanafunzi. Wanafunzi wengi hujisikia vizuri zaidi kushiriki katika shughuli za darasani zinazoambatana na mbinu za kusifu, matumizi mazuri ya imoji, utoaji wa zawadi, ushajihishaji pamoja na vifaa vya kufundishia kama picha, chati, na vifaa vyengine vya kujifunzia. Mambo yote hayo huwapa hisia wanafunzi kwamba kujifunza lugha lengwa ni rahisi na ni lugha ya kufurahisha.

Halikadhalika, kuwapa wanafunzi fursa ya kutoa mawazo yao na kukubali kuwa makosa katika kujifunza lugha ya kigeni ni jambo la kawaida. Vilevile, kutoa mrejesho chanya kwa wanafunzi huimarisha ujifunzaji unaoleta mafanikio mazuri. Korb (2012) anaeleza kuwa kutoa mrejesho ni njia mojawapo ya kukidhi haja ya mafanikio. Aidha, kumsifia mwanafunzi wakati wa kujifunza kunamjenga ajiamini na awe na umahiri. Reeve (2001) anafafanua kwamba mwanafunzi anahitaji kupewa mrejesho kama amefanya vizuri. Kufanya hivyo kunaweza kuongeza kuridhika kwa wanafunzi na kujihimiza kwa kuongeza bidii na kujitathmini. Hivyo, makala hii imechunguza aina na mbinu za utoaji motisha ya nje zinazotumika wakati wa ufundishaji Kiswahili kwa wageni.

**2.0 Maelezo kuhusu dhana mbalimbali**

Istilahi muhimu zinazohusiana na makala hii ambazo zimefafanuliwa kwa upana katika sehemu hii ni motisha, motisha ya nje, lugha ya kigeni na ufundishaji wa lugha ya kigeni.

**2.1 Motisha**

Motisha ni kichocheo cha ndani kinachomsukuma mtu kufanya kitu ili kufikia malengo yaliyowekwa (Harmer, 1991). Motisha inaweza kuwa ni moja ya sehemu au sababu za mchakato wa kujifunza lugha ya pili ama ya kigeni. Wade na Tavris, (1998) wanatilia mkazo kwa kueleza kuwa motisha ni mchakato unaoingizwa ndani ya mtu ambao husababisha kiumbe hicho kuelekea kwenye lengo halisi lililokusudiwa. Motisha katika ujifunzaji huongeza ari na hamu ya kujifunza lugha kwa wanafunzi wanaotarajia kuongeza ufanisi katika lugha anayojifunza.

**2.1 Motisha ya nje**

Motisha ya nje ni ile ambayo mwanafunzi hutegemea kupata, kusikia au kuona kitendo kinafanyika kama vile kufaulu mtihani au kupata tunzo za kifedha ama zawadi ambayo itamwezesha kupata hamu ya kuendelea kujifunza lugha na kufikia malengo aliyokusudia. Dornyei (2001) anaieleza motisha ya nje ni kitendo kinachofanywa ili kufikia malengo fulani, kama vile kupata zawadi au kuepuka adhabu.

**2.3 Lugha ya kigeni**

Lugha ya kigeni ni lugha ambayo wazungumzaji wake wako nje ya eneo halisi la wazawa. Mtesigwa (2009) anaeleza lugha ya kigeni kuwa ni lugha ambayo mtu hujifunza na kuitumia lakini wazungumzaji wa lugha hiyo wako nje ya nchi au jamii anakokaa mwanafunzi huyo.

**2.4 Ufundishaji wa lugha ya kigeni**

Kwa mujibu wa Moeller na Catalano (2015) ufundishaji wa lugha ya kigeni ni kufundisha lugha ambayo haitokani na wazawa wa sehemu inayohusika. Hivyo, ufundishaji wa lugha ya kigeni hurejelea kumfundisha mtu asiye mzaliwa wa mazingira ya lugha anayozungumza kawaida.

## 3.0 Aina za motisha ya nje

Kabla ya kufanya utafiti huu mtafiti alikuwa anajua kwamba motisha ni jambo la kawaida wakati wa ufundishaji. Vilevile, hakuweza kutafautisha motisha ya ndani na motisha ya nje. Baada ya utafiti wa kina na kuchunguza walimu wanapofundisha mwandishi wa makala hii aligudua kuwa kuna aina kuu mbili za utoaji wa motisha ya nje wakati wa ufundishaji Kiswahili kwa wageni. Utoaji wa motisha ya nje zinazotumia maneno na motisha ya nje zinazotumia vitendo. Motisha hizi hutolewa kwa maneno peke yake au vitendo tu ama kuambatanisha maneno na vitendo. Pia motisha za maneno hutumika darasani na kwenye kazi za wanafunzi wanazoandika katika vitabu vyao. Motisha za vitendo hufanyika darasani na nje ya darasa. Wakati mwengine motisha za vitendo huchorwa katika kazi za wanafunzi kwa kutumia mfanano wa imoji. Imoji ni vipicha vidogovidogo vinavyotoa taswira ya jambo linalipendeza au linalochukiza na mengineyo. Mwandishi wa makala hii ameweza kuzing'amua motisha hizo na kuweza kuzifafanua ili watoaji wa motisha waweze kuzitumia ipasavyo.


**3.1 Motisha ya nje zinazotumia maneno**

Utoaji motisha ya nje zinazotumia maneno hutolewa wakati wa mazungumzo au maandishi. Mwalimu anapofundisha hutumia motisha ya nje zinazotumia maneno tafauti kwa wanafunzi

wanaojaribu au kujibu vizuri. Hutumia maneno yanayowatia hamasa wakati wa kujifunza kwa kuwaambia nzuri, nzuri sana, mashaallahu, hongera, haijambo, umefanya vizuri, endelea na sawa. Utoaji wa motisha ya nje zinazotumia maneno hutolewa kwa wanafunzi wote ili wapate hamasa na wajisikie huru wanapojifunza Kiswahili. Mtafiti alipokuwa darasani alibaini kuwa maneno hayo huwa na uzito tafauti katika utoaji wa motisha. Kwa mfano, mwalimu anapotumia neno nzuri humaanisha mwanafunzi amefanya jambo la kupendeza. Ikiwa mwanafunzi amefanya jambo la kupendeza zaidi huambiwa nzuri sana. Vilevile, neno hongera hutolewa pale mwanafunzi anapoutumia msamiati mpya katika mazungumzo au maandishi ama kusoma habari kwa usahihi. Neno mashaallahu mara nyingi hutolewa katika stadi ya kuzungumza na kusoma ikiwa mwanafunzi ameweza kasoma habari vizuri. Aidha neno haijambo hutumika katika kiwango cha wastani pale mwanafunzi anapojaribu kujibu maswali, kusoma habari na hata kuandika katika kiwango cha kuridhisha. Halikadhalika, neno sawa hutumika pale mwanafunzi anapofanya zoezi la kuelezea kitu na kuonekana kuwa ana wasiwasi juu ya anachokielezea, mwalimu husema neno sawa ili kumpa moyo mwanafunzi asisitesite wakati wa kuelezea jambo. Hivyo, ni dhahiri kuwa utoaji wa motisha zinazotumia maneno wakati wa kujifunza huwashajisha wanafunzi wageni kuipenda lugha ya Kiswahili. Motisha zinazotumia maneno huwatia ari na kuwafanya wanafunzi wawe huru wanapojieleza au wanapofanya mazoezi mbalimbali darasani.

### 3.2 Motisha ya nje zinazotumia vitendo

Motisha za nje zinazotumia vitendo mara nyingi huambatana na matumizi ya viungo vya mwili. Utoaji wa motisha za aina hii hutolewa ili kuwatia wanafunzi hamasa ya kujifunza Kiswahili. Mtafiti alipokuwa darasani aligundua kwamba ufanyaji wa vitendo mbalimbali vya uhamasishaji wakati wa ufundishaji huwafanya wanafunzi kuwa wachangamfu na kuwa karibu na mwalimu. Vitendo hivyo ni pamoja na kupiga kofi, kutabasamu, kugonga meza, nipe tano na kutikisa kichwa. Ufanyaji wa vitendo hivyo huwatia shauku wanafunzi wakati wa kujifunza Kiswahili ambapo hujifunza kwa urahisi na upendo. Mtafiti alimshuhudia mwalimu akipiga kofi baada ya mwanafunzi kuweza kusoma habari vizuri katika gazeti wakati wa ufundishaji kama inavyojionesha picha ifuatayo:



**Chanzo:** Uwandani, (2021)

Kwa ujumla njia nzuri ya utoaji motisha ya nje zinazotumia maneno na vitendo kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa wageni ni wakati wa tendo la ufundishaji likiwa linaendelea kwasababu huwatia moyo wanafunzi na kuwaongezea shauku ya kujifunza zaidi.

**4.0 Mbinu zinazotumika katika utoaji motisha ya nje**


Mtafiti katika uchunguzi wake alioufanya darasani alibaini kwamba kuna mbinu nne kuu zinazotumika wakati wa utoaji wa motisha ya nje kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa wageni. Mbinu ya kuwasifu wanafunzi, kutumia imoji, kutoa zawadi na kuwashajihisha wanafunzi.

**4.1 Mbinu ya kuwasifu wanafunzi.**

Walimu wanapofundisha hutumia mbinu mbalimbali zinazoambatana na utoaji wa motisha. Mbinu mojawapo ya motisha ni kuwasifu wanafunzi wakati tendo la kufundisha linaendelea. Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) kusifu ni kitendo cha kuelezea hali ya kupendeza kwa jambo, kitu au mtu. Kwa kawaida mbinu ya kuwasifu wanafunzi hufuatana na motisha ya maneno ambayo wanafunzi wakiyasikia hufarijika sana na kujifunza kwa utulivu. Maneno ambayo hutumika mara kwa mara kuwasifu wanafunzi ni nzuri, nzuri sana, hongera, umefanya vizuri, mashaalahu na nyengine. Wanafunzi wanaposifiwa kwa kufanya vizuri na kutambua kuwepo kwao huongeza bidii ili wasifiwe zaidi na zaidi.

Mbinu hii ya kuwasifu wanafunzi ina faida kubwa katika tendo la kujifunza. Huwafanya wanafunzi waweze kujifunza kwa urahisi, kupata hamu, ari na hamasa ya kuendelea kujifunza muda wote. Pia, huwajengea wanafunzi kumbukumbu ya kudumu, huwajenga wanafunzi kuwa washindani katika mafunzo yao. Vilevile, kuimarisha uhusiano mzuri kati ya mwalimu na mwanafunzi na kuwaondolea woga wanafunzi na kuwajenga katika kujaribu na kutoa jawabu kutokana na hisia zao. Kwa mujibu wa Jafari (2013) alieleza kuwa mbinu ya kuwasifu wanafunzi huwasaidia kutumia akili zao vizuri.

Hivyo, faida zinazopatikana katika kuwasifia wanafunzi huwasaidia kuchangamsha akili na kutanua upeo wa fikra zao.
Kwa mfano mwandishi katika uchunguzi wake alimbaini mwalimu mmoja kati ya walimu aliowafanyia uchunguzi kwa kumwambia mwanafunzi achague neno sahihi katika mabano na kujaza nafasi zilizowazi kwa kutumia kauli ya kutendeka. Baada ya mwalimu kuridhishwa na kazi ya mwanafunzi kwa kupatia jawabu zote alimsahihishia na kumwekea neno nzuri sana. Mwanafunzi baada ya kuona neno hilo katika kazi yake alifurahi sana na kuomba aongezewe kazi nyengine. Uthibitisho wa motisha ya maneno ambayo huandikwa katika kazi za wanafunzi baada ya usahihishaji ilijidhihirisha katika kielelezo kifuatacho cha kazi ya mwanafunzi:


Zoezi la tatu:

Chagua kitenzi sahihi kisha jaza katika sehemu iliyo wazi katika utendeka.

( pika, elewa, pita, fahamu, shona )

1. Chakula Kimepikika vizuri. Nimekula mpaka nimevimbiwa.
2. Somo la leo limefahamika vizuri sana
3. Barabara ya Mkunazini inapitika hata wakati wa mvua.
4. Nguo yake imeshoneka vizuri.
5. Maelezo ya mwalimu yameeleweka vizuri

Nzuri Sana


**Chanzo:** Uwandani, (2021).

Hata hivyo, mbinu hii inaweza kusababisha changamoto ikiwa mwalimu hatoitumia kwa umakini. Miongoni mwa changamoto zinazoweza kujitokeza ni pamoja na kudumaza vipaji vya wanafunzi; baadhi ya wanafunzi wanaweza kushindwa kujaribu pindipo wakiwa darasani kwa kujiona wao wana uwezo mdogo wa kufikiri na kutopatia jawabu analolitarajia mwalimu. Pia wanafunzi wanaweza kuoneana choyo, ikiwa kuna mwanafunzi atakuwa anapatia jawabu na mwalimu kumsifu mno mwanafunzi huyo. Hali hii huleta muono hasi kwa wanafunzi ambao hawasifiwi mara nyingi, na kusababisha choyo kutawala miongoni mwa wanafunzi hao.
Kwa ujumla, utoaji wa motisha ya nje kwa kutumia mbinu ya kuwasifu wanafunzi waonajifunza Kiswahili kwa wageni ni nzuri sana na ni rahisi kutekelezeka kwasababu motisha hiyo hutolewa kwa njia ya matamshi au kwa vitendo wakati wa kusahihisha kazi zao.

**4.2 Mbinu ya kutumia imoji**


Mtafiti alipofanya uchunguzi aligundua kwamba walimu wanatumia mbinu ya vitendo vinavyoshabihiana na imoji wakati wa ufundishaji Kiswahili kwa wanafunzi wageni. Miongoni mwa vitendo vinavyoshabihiana na imoji wanazozitumia ni dole gumba na uso wenye furaha. Pia hutumia mchoro wa nyota ama picha ya nyota kuweka katika kazi au katika mkono wa mwanafunzi kama ni ishara ya kupiga hatua ya jambo analolifanya. Imoji hizo humaanisha uzuri wa kazi iliyofanywa na wanafunzi. Walimu hutumia imoji ili kuwafanya wanafunzi wafurahie tendo la kujifunza na

waipende lugha wanayojifunza. Mbinu hii hutumika wakati wa mazungumzo na wakati wa kitendo cha usahihisahji wa kazi za wanafunzi. Imoji zinazotumika wakati wa mazungumzo ni kiganja cha mkono kinachoonesha dole gumba ambacho kinamaanisha kuwa mwalimu anakubaliana na jawabu ya mwanafunzi aliyoitowa wakati wa mazungumzo. Picha ifuatayo inathibitisha namna walimu wa Kiswahili kwa wageni wanavyotumia imoji ya dole gumba katika kutoa motisha inayoonekana kwa wanafunzi wao baada ya kuweza kujibu maswali vizuri, kusoma habari kwa usahihi na hata kujaribu kufanya mazungumzo kwa pamoja. Tizama picha ifuatayo:



**Chanzo:** Uwandani, (2021).

Pia wakati mwengine, walimu hutumia imoji ya uso wenye bashasha na picha ama mchoro wa nyota wakati wa usahihishaji wa kazi za wanafunzi walizoandika kwa lengo la kuwahamasisha katika ufanyaji wa kazi zao, hali hiyo huwafanya wapende kujifunza Kiswahili zaidi. Baadhi ya imoji zinazotumika katika usahihishaji wa kazi za wanafunzi ni uso wenye furaha na mchoro wa nyota. Walimu hutumia imoji hizo baada ya wanafunzi kuweza kufanya kazi za uandishi vizuri kama vile, kuandika mazungumzo yanayohusiana na mada maalumu, kutunga sentensi na mambo mengine. Mwalimu hutumia imoji ya uso wenye bashasha akimaanisha kuwa mwanafunzi amepatia jawabu katika kazi yake aliyofanya. Kielelezo kifuatacho kinathibitisha matumizi ya imoji ya uso wenye furaha ambao mwalimu huweka mwisho wa kazi ya mwanafunzi iliyosahihishwa:




Je umewahi kusikiliza muziki hapa Zanzibar? Kama ndio elezea umejifunza nini katika muziki huo.

Ndio, nilisikiliza muziki wa Taarab hapa Zanzibar katika darasa. Niliifunza muziki wa Taarab ni kuhusu mada nyingi tofauti: nyimbo ya mpenzi au muziki ni burudani, starehe, na furaha. Nilisikiliza muziki wa Prince Kioo. wimbo wake unaitwa upendo. wimbo unahusu upendo wa Mungu. wimbo unasema "Ee Mungu wewe ni nguvu yetu, ilete baraka kwetu sisi wanawako, Haki yako ewe ni nguvu yetu, uwe faraja yetu hata kwa machungu. Upendo na amani tujazie, Undugu uzidi uhasama na kisasi Mbona majirani tunapigana? Tufunze upendo tukakumbatiane"

**Chanzo: Uwandani**, (2021).

Pia, walimu huchora nyota moja au zaidi, zenye kuonesha hatua ya maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza. Mtafiti alimshuhudia mwalimu akisahihisha kazi ya mwanafunzi na baada ya kupatia jawabu zote, alimuekea mchoro wa nyota kwa kumpa motisha kwa kazi nzuri aliyoifanya. Uthibitisho wa utumiaji wa imoji ya nyota katika kazi za wanafunzi zilizosahihishwa unajidhihirisha katika kielelezo kifuatacho:



Mazoezi:

Jaza nafasi zilizowachwa wazi kwa kutumia njeo ya wakati uliopita na wakati ujao **(li/ta).**

1. John a.ta.rudi Zanzibar wiki ijayo
2. Mimi ni.li.anza kujifunza Kiswahili tangu mwaka 2020
3. Tu.li.kwenda kutembelea shamba la viungo Jumatano iliyopita
4. Jumapili ijayo ni.ta.kwenda kanisa la Chuwini.
5. Jana tu.li.jifunza mada ya njeo

7/6/2021

**Chanzo:** Uwandani, (2021).

Miongoni mwa faida zinazopatikana katika utumiaji wa mbinu ya imoji ni kuwafanya wanafunzi wafurahie tendo la kujifunza na waipende lugha wanayojifunza. Vilevile, husaidia kuwahamasisha wanafunzi kujaribu zaidi na zaidi wakiwa darasani na hata nje ya darasa. Hivyo, mwalimu hutumia imoji hizo ili kuwapa wanafunzi wake motisha inayoonekana kwa vitendo baada ya wanafunzi hao kujaribu au kupatia jawabu vizuri. Mfano kusoma habari kwa usahihi, kujibu maswali, kutunga

sentensi na hata kutaja msamiati mpya walioupata kwa marafiki wa lugha. Hali hii huwafanya wanafunzi wawe karibu zaidi na mwalimu, hivyo ujifunzaji wao huwa rahisi zaidi.
Hata hivyo, mtafiti alibaini kuwa baadhi ya walimu hawana mwamko wala taaluma nzuri ya kutumia mbinu ya imoji katika kuwapa motisha wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa wageni. Kwa ujumla mwandishi alibaini kuwa wanafunzi wageni wanapenda sana na kufurahiya zaidi matumizi ya mbinu ya imoji kuliko mbinu nyengine.

**4.3 Mbinu ya kutoa zawadi**

Mbinu nyengine ya motisha ya nje inayotumiwa na walimu ni utoaji wa zawadi wakati wa ufundishaji Kiswahili kwa wageni. Land na Zafar (2016) wanasisitiza kwamba motisha ya nje inahusu mazingira ya pesa, chakula na zawadi. Mbinu hii huwawezesha wanafunzi kujifunza kwa furaha. Kwa kawaida wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa wageni hupewa zawadi ya vitu ambavyo vitawashajihisha na kuwatia hamasa zaidi ya kujifunza Kiswahili. Mtafiti alipokuwa anafanya uchunguzi darasani alishuhudia zawadi zinazotolewa za vinywaji kama soda, maji, kahawa na dafu, pia, alipata kuona zawadi za vyakula kama urojo na ubuyu pamoja na vifaa vya kujifunzia wakati wa ufundishaji; kama CD na vipeperushi vinavyohusiana na mada.

Motisha ya utoaji wa zawadi kwa wanafunzi una faida nyingi sana. Zawadi huwafanya wanafunzi kuwa karibu zaidi na walimu, kama inavyofahamika kuwa tendo la kupeana zawadi hujenga upendo baina ya mtoaji na mpokeaji, huwafanya wanafunzi wafurahie usomaji ambapo hulifanya darasa kuwa hai muda wote, walimu wanapotoa motisha ya zawadi huwahamasisha wanafunzi kuendelea kujifunza Kiswahili katika taasisi yao pamoja na kuitangaza taasisi hiyo katika mataifa mbalimbali. Hoja hii inaungwa mkono na Jafari (2013) ambaye anasisitiza kuwa utoaji wa zawadi ni mbinu nzuri katika kutoa motisha kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya kigeni.

Hata hivyo, utumiaji wa mbinu hii unaweza kuleta baadhi ya changamoto kwa walimu kwa kutumia gharama za kifedha katika kuzipata zawadi hizo. Mfano, zawadi kama CD, kanga, dafu na vyenginevyo hutumia gharama za fedha kuvinunua vitu hivyo. Pia, muda mwingi unapotea kwa ajili ya kuvitayarisha vitu hivyo. Halikadhalika ikiwa mwalimu atatoa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri tu itapelekea wanafunzi wenye uelewa mdogo kuvunjika moyo na kuchukia ufundishaji wa aina hiyo.

**4.4 Mbinu ya pongezi ya kuwashajihisha wanafunzi**

Mwandishi aligundua kuwa kuwapongeza wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa wageni ni miongoni mwa mambo yanayowashajihisha wakati wa kujifunza. Kuwashajihisha wanafunzi kwa kutoa pongezi ni tafauti kidogo na ile mbinu ya kuwasifu wanafunzi. Kuwasifu wanafunzi ni kutumia maneno tu ya kuwapa motisha lakini kuwapongeza wanafunzi ni kutumia vitendo ama mwambatano wa maneno na vitendo.

Pongezi hizi za kuwashajihisha wanafunzi aghalabu hutolewa ndani ya darasa na nje ya darasa. Pongezi za ndani ya darasa hutolewa pale mwalimu anapowasilisha somo lake akiwa darasani kwa kupiga kofi au alama ya nipe tano (ni mkono wa kulia wa mwalimu na mwanafunzi wanayoigongesha ikiwa imefungwa ngumi). Matendo haya hufanywa na mwalimu pamoja na mwanafunzi wake. Pia mwalimu kumchagua mwanafunzi anayefanya vizuri kuwa kiongozi ikiwa ni pongezi zinazostahili kwa mwanafunzi huyo.

Kwa upande wa pongezi zinazotolewa nje ya darasa, tendo hili hufanyika kwa mwalimu anapomaliza kufundisha mada yake kwa ukamilifu na kuwatathmini wanafunzi hao kwa kuridhika na ufanisi wao, walimu huwatoa wanafunzi nje ya darasa kwa ajili ya kuwapa motisha wanafunzi wao wanaojifunza Kiswahili. Mfano wa pongezi za nje ya darasa kama kwenda matembezi ya hiari ambayo hayamo katika ratiba za ziara za kimasomo. Pongezi hizi huwafanya wanafunzi kupenda safari zaidi kuliko kukaa darasani kwasababu matembezi hayo husaidia kuona uhalisia, kuvutiwa, kuonja, kugusa na kunusa vitu mbalimbali vilivyo nje ya darasa. Hali hii huwafanya wanafunzi wajitahidi katika kujifunza ili wapate fursa hiyo.

Mbinu ya kuwapongeza kwa kuwashajihisha wanafunzi ni nzuri katika utoaji wa motisha ya nje kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa wageni kwasababu huwafanya wanafunzi kuifurahia lugha wanayojifunza. Hivyo, ni vyema walimu wanaofundisha Kiswahili kwa wageni waongeze jitihada ya kutoa motisha kwa kutumia mbinu ya kuwapongeza wanafunzi ili kuleta ufanisi mzuri kwa wanafunzi katika taasisi hiyo.

Kwa ujumla utumiaji wa mbinu hizi za utoaji wa motisha ya nje unaofanywa na walimu huwafanya wanafunzi waongeze juhudi katika kujifunza lugha. Hali hiyo hupelekea ufanisi katika upatikanaji wa lugha ya Kiswahili.

**5.0 Hitimisho**

Mtafiti alipofanya uchunguzi kuhusu aina na mbinu za utoaji wa motisha ya nje aligundua kuwa utoaji wa motisha ya nje una umuhimu mkubwa katika ufundishaji Kiswahili kwa wageni. Iwapo wanafunzi watafundishwa vizuri na kupewa motisha kwa wingi, itasababisha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi watakaojifunza Kiswahili katika idara ya Kiswahili kwa wageni na kupata ongezeko la mapato hususan fedha za kigeni. Mwisho mwandishi wa makala hii anawashauri walimu wanaofundisha Kiswahili kwa wageni wazidishe juhudi katika kutoa motisha zinazoonekana na utumiaji mzuri wa mbinu za uhamasishaji, pia kubuni mbinu nyengine ambazo zitaleta tija kwa wanafunzi na taasisi husika.

**Marejeleo:**

- Alhodiry, A. (2016). The Libyan Teacher's Role in Developing Students Motivation. *International Conference on Teaching and Learning English as an Additional Language*. (232), 83- 89.
- Anjomshoa, L., & Sadighi, F. (2015). The Importance of Motivation in Second Language Acquisition. *International Journal on Studies in English Language and Literature*. 3(2), 126- 137.
- BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Borah, M (2021). Motivation in Learning. *Critical Review*. 8: 02, 2021
- Gardner, R. (2010). *Motivation and Second Language Acquisition*: The socio-educational model. Peter Lang Publishing
- Harmer, J. (1991). *The Practice of English Language Teaching*. Longman. Pearson Education Limited
- Jafari, S. (2013). Motivated learners and their success in learning a second language. *Theory and practice in language study*. 3(10), 1913-1918.
- Korb, K. (2012) Creating a Classroom Environment that Fosters Positive Motivation in the Nigerian Context.The Nigeriaan Educational Psychologist 10,221-230
- Land, S., & Zafar, S. (2016). Motivation in second language learning: A Retrospect. *International interdisciplinary research journal*. 4 (1) 7- 13.
- Moeller, J., & Catalano, T. (2015). Foreign Language Teaching and Learning. *Journal of International Encyclopedia for Social and Behavioral Sciences*. 9 (2), 327-332.
- Mtesigwa, C. K (2009). Utayarishaji wa Vitabu vy Kufundishia Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Haja ya Kuzingatia Mkabala wa Mawasiliano. *Kiswahili* 72(1), 52-67.
- Reeve, J. (2001). *Understanding Motivation and Emotion* (3rd ed). New York: John Wiley & Son
- Reeve J. & Halusic, M. (2009) How K 12 Teachers can Put Self Determination Theory Principle into Practice. *Theory and Research in Education* 7,145-154
- Wade, C., & Tavris, C. (1998). *Psychology*. New York: Addison-Wesley Educational Publishers.